

**JIFUNZE KUHUSU
KILE WAMISIONARI
WANACHOFANYA!
KISHA FUATA NJIA
NA UKABILIANE NA
CHANGAMOTO.**

CHANGAMOTO YA UMISIONARI



Wamisionari hukutana na watu na kuzungumza nao.

Fikiria kuhusu talanta uliyo nayo. Kisha tumia talanta hiyo kumtumikia mtu!



Jifunze kusema maneno machache kwa lugha nyingine. Unaweza kujifunza kusema, "Yesu ananipenda" au "Mimi ni mwana wa Mungu."



Baadhi ya wamisionari hujifunza lugha mpya.



Wamisionari hushiriki talanta zao! Baadhi hupiga piano kanisani, hujifunza maandiko ya kushiriki au hutumia talanta zingine kwa ajili ya kuwabariki wengine.



Pata kumjua mtu katika darasa lako au ujirani wako ambaye humfahamu.



Wamisionari huwafunza wengine kuhusu Yesu Kristo.



Wamisionari husali kwa ajili ya wengine.



Wafikirie watu wawili au watatu unaowajua na sali kwa ajili yao. Muombe Baba wa Mbinguni awabariki.



Mwambie rafiki au mwanafamilia jambo ulilojifunza kuhusu Yesu katika Msingi.



VIELEZO NA SAMMIE FRANCIS